

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

SURA 288

SHERIA NDOGO

Zimetungwa Chini ya Kifungu cha 89

SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII - TIBA KWA KADI) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO, 2010

lina na  
mwanzo wa  
kutumika

Matumizi

Tafsiri

1 Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Uanzishaji Mfuko wa Afya ya Jamii - Tiba kwa Kadi) (TIKA) za Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, 2010 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye gazeti la serikali.

2 Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

3 Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakopozwa vinginevyo,

“Ada ya mtumiaji” maana yake ni ada inayotozwa na Hospitali, Kituo cha Afya au Zahanati, kwa ajili ya Huduma ya Afya iliyotolewa kwa mtumiaji.

“Asasi” ni pamoja na shule, vyuo, vikundi mhalimbali vilivyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria au Asasi yoyote itakayokuwa imekubaliwa na kuidhinishwa na Bodi.

“Bodi” maana yake ni Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri iliyoungwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288.

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

“Huduma za Afya” maana yake ni huduma zote za afya zinazotolewa na Hospitali wa Serikali na watu binafsi na zinajumuisha huduma nyingine za afya zilizoanzishwa kwa madhumuni ya kutoa huduma za afya ikiwa ni pamoja na Vituo vya Afya na Zahanati.

“Kadi” maana yake ni kadi itakayotolewa na Bodi kwa mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

“Kaya” maana yake ni:

(a) mama, Baba na watoto wenye umri chini ya miaka kumi na minane;

(b) mwanachama yeyote aliyefikia umri wa miaka kumi na minane au zaidi na awe na mtoto au bila mtoto mwenye umri chini ya

